**OR-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**
**SHULE YA SEKONDARI MIKUMI S.L.P. 80, MIKUMI**

**Barua Pepe: mikumisecondary92@yahoo.com SIMU: 0658609050**

**…./…../2020**

**Kumb. Na: MKM.SS/ADM/2021/01**
**Jina la Mwanafunzi: ………………………………………………………………………**
**S.L.P. ………, …………………………….**

**Ndugu,**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIKUMI WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mikumi. Shule ipo umbali wa kilomita moja na nusu kutoka stendi kuu ya Mji Mdogo wa Mikumi, barabara ya kuelekea Kilombero. Muhula wa masomo unaanza 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/ 01/ 2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 11/02/2021.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za shule

### A. WAVULANA

i. Suruali mbili za kijani **zisizobana** (**Modal**) zenye marinda manne mbele, mfuko mmoja wa nyuma na "belt hooks" za mkanda ziwe nyembamba za kawaida, **iwe na pindo chini (turn up), upana wa chini size 15**
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyobana.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili.
v. Nywele fupi zisizo na mtindo, zisizidi nusu sentimeta.
vi. Tai na fulana (T-shirt).
vii. Track suit ya kijani yenye mistari miwili myeupe pembeni, fulana nyekundu na raba kwa ajili ya vipindi vya michezo.
viii. **Angalizo: Nimarufuku kuvaa suruali za kubana *(modal)*** . .(***k****ama hujayaelewa haya maaelekeza tafadhali fika shuleni uoneshwe jinsi suruali inavyotakiwa kuwa, kinyume na maelekezo haya mtoto hatapokelewa*)

### B. WASICHANA

i. Sketi mbili za kijani zinazovuka magoti zenye rinda kubwa mbele na nyuma, marinda mawili mawili yanayotazamana; mkanda (belt) usiwe mpana.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyobana.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu
iv. Soksi nyeupe jozi mbili zisizokwa na rangi nyingine wala pambo lolote.



Scanned with CamScanner

v. Nywele fupi zisizo na mtindo, zisizidi nusu sentimeta.
vi. Tai na fulana (T-shirt).
vii. Hijabu nyeupe isiyo na urembo wowote ***(hijabu zivaliwe na sketi ndefu na mashati ya mikono mirefu, na hairuhusiwi kusuka nywele).***
viii. Trucksuit nyeusi, fulana nyekundu na raba kwa ajili ya vipindi vya michezo.

**2.2 Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:**

i. Madaftari makubwa (counter books) 12, kalamu za wino za kutosha.
ii. Rula nyeupe ya kuangaza ya futi moja, mkebe (mathematical set) wa hesabu.
iii. Vitabu vya kiada kwa masomo yote (Uraia, Historia, Jiografia, Kiswahili, Kingereza, Fizikia, Kemia, Baiolojia, Tehama na Hisabati).
iv. Picha mbili (2) za rangi za passport size zenye kivuli cha rangi ya blue bahari nyuma, mwanafunzi apige akiwa amevaa shati jeupe.

**2.3 Vifaa vya usafi**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vya usafi na vikabidhiwe shuleni siku ya kuripoti kwa mchanganuo ufuatao:

a. **Wasichana:** Ndoo moja ndogo ya kuchotea maji, fyekeo moja na ufagio mmoja wa chelewa.
b. **Wavulana:** Jembe moja lenye mpini imara na ufagio mmoja wa chelewa.

**2.4 Hostel kwa wasichana**

Nafasi ya kuishi hostel inapatikana kwa wanafunzi wa kike tu. Hata hivyo nafasi kwa anayehitaji awasiliane na Mkuu wa Shule kwa namba tajwa hapo juu ili kujua gharama na taratibu nyinginezo.

**3.0 SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na taratibu za shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira pia.



Scanned with CamScanner

g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa.
i) Kutunza mali za umma.

### 3:1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi
b) Uasherati, ushoga na ubakaji.
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
d) Kupigana au kupiga.
e) Kudharau bendera ya taifa.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya uma.
g) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
h) Kuoa au kuolewa
i) Kutoa mimba na kutia mimba.
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kuwa na simu ya mkononi.

### 4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a. Medical examination form, ijazwe na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutokushiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria za shule.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

..........................
**MKUU WA SHULE**
THE HEADMASTER
MIKUMI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 80
MIKUMI



Scanned with CamScanner

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**
**SHULE YA SEKONDARI YA MIKUMI, S.L.P. 80, MIKUMI**

---

| Picha ya rangi ya Mwanafunzi yenye kivuli cha blue bahari nyuma |
|---|

## TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina: ...................................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa: ........./ ........../....................... (taja siku, mwezi na mwaka)**.
3. Kabila: ...........................................
4. Taifa: ............................................
5. Dini: .................................... Dhehebu: ...............................................
6. Jina la Baba: ........................................................................................................
7. Anwani ya Baba: ..................................................................................................
   ..................................................................................................
   ..................................................................................................
8. Kazi ya Baba: ......................................................................................................
9. Jina la Mama: ......................................................................................................
10. Anwani ya Mama: ................................................................................................
    ................................................................................................
    ................................................................................................
11. Kazi yake: ..........................................................................................................
12. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana:...........................................................
13. Jina na anwani ya Mlezi wako (kama si Mzazi):

    .......................................................................................................................
    .......................................................................................................................
    .......................................................................................................................
    .......................................................................................................................

    Ninathibitisha kwamba habari zote nilizotoa ni kweli na Sahihi

    Sahihi ya Mwanafunzi: ......................................... Tarehe: ....................

    Sahihi ya Mzazi/Mlezi: ......................................... Tarehe: ....................

14. Jina na sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji: ....................................

| MHURI |
|---|

** Mwanafunzi aje na kivuli cha nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**NB: Endapo mwanao anatatizo lolote linalohitaji uangalizi wa kipekee, mzazi/mlezi unashauriwa kutoa taarifa shuleni wakati unamleta mwanao siku ya kuripoti**



Scanned with CamScanner

**Sehemu ya Mwanafunzi**

Mimi: ............................................................ (Jina) Msichana/Mvulana ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka 2021 katika Shule ya Sekondari Mikumi na nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za Nchi.Nitakuwa Mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za elimu ya kujitegemea.

**Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi ................................................................ ambaye ......................... (uhusiano) ninakubali mtoto wangu kuingia Shule ya Sekondari ya Mikumi kidato cha kwanza mwaka 2018 na ninaahidi kumpatia mahitaji yote kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na Shule ( Joining Instructions) na ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na Shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa Shule na Taifa kwa ujumla.

Anwani yangu ya kudumu ni:

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

Namba ya simu ya mkononi ................................ ya mezani/ofisini..............................

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi yaliyothibitishwa na Mkuu wangu wa Idara au Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata/Kijiji.

Sahihi: ............................................. Tarehe: ...............................

**Jaza fomu hii na kuirudisha shuleni wakati wa kuripoti.**



Scanned with CamScanner

## FOR MEDICAL EXAMINATION

**From:** The medical officer
.........................................
.........................................
.........................................

To: The Head of School
Mikumi Secondary School
P.O Box 80,
Mikumi

### RE: MEDICAL CERTIFICATE FORM

(To be completed by a Medial Officer in respect of all Form I entrants)

1. Pupil's full name..................................................................................................
2. Age: ..........years
3. Sex: ............................

| EXAMINATION AREA | REMARKS |
|---|---|
| i. Blood count (Red and white) | |
| ii. Stool Examination | |
| iii. Syphilis and other venereal diseases test | |
| iv. T.B. Test | |
| v. Eye Test | |
| vi. Ears | |
| vii. Spleen | |
| viii. Abdomen | |
| ix. Urine for plasma test | |
| x. Test for pregnancy (for girls only) | |

**ADDITIONAL INFORMATION**

(If any) e.g. physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases, etc
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................

I certify that the above **is fit/ is not fit** to pursue studies in Secondary Education.

Station: ......................................  Designation: ....................

Signature: ..............................................  Date: ...............................

Official stamp



Scanned with CamScanner